BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2015

## 021 KISWAHILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2015

# 021 KISWAHILI

Kimechapishwa na
Baraza la Mitihani la Tanzania
S.L.P. 2624, Dar es Salaam
Tanzania

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2016**

Haki zote zimehifadhiwa

# YALIYOMO

DIBAJI.......... iv
1.0 UTANGULIZI.......... 1
2.0 TATHIMINI KWA KILA SWALI .......... 2
2.1 Sehemu A: Ufahamu.......... 2
2.1.1 Swali la 1: Ufahamu .......... 3
2.2 Sehemu B: Matumizi ya Lugha na Usahihi wa Maandishi .......... 7
2.2.1 Swali la 2: Usahihi wa Tungo na Rejesta .......... 7
2.3 Sehemu C: Sarufi .......... 12
2.3.1 Swali la 3: Aina za Maneno na Uambishaji .......... 12
2.4 Sehemu D: Fasihi Simulizi .......... 17
2.4.1 Swali la 4: Fasihi Simulizi.......... 17
2.5 Sehemu E: Uandishi wa Insha/Utungaji. .......... 22
2.5.1 Swali la 5: Uandishi wa Barua za Kirafiki .......... 22
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KWA MADA .......... 26
4.0 HITIMISHO .......... 27
5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO.......... 27
KIAMBATISHO A .......... 28
KIAMBATISHO B.......... 29

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa taarifa kuhusu uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Upimaji wa Kidato cha Pili katika somo la Kiswahili. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu wa somo hilo kwa wanafunzi, walimu, wazazi, watunga sera na jamii kwa ujumla.

Taarifa hii ni tathmini ya kati ambayo inaonesha mafanikio au upungufu kadhaa uliobainika katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi waliopimwa wa Kidato cha Pili mwaka 2015. Aidha, majibu ya wanafunzi ndio msingi wa yale yote ambayo mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuyatoa kwa wanafunzi katika elimu ya Sekondari kwa Kidato cha Pili.

Uchambuzi huu unalenga kuonesha sababu za wanafunzi kufanya vizuri au vibaya katika upimaji wa Kidato cha Pili. Aidha, taarifa inaonesha kuwa sababu zilizowafanya wanafunzi kupata alama za juu katika majibu ya maswali mbalimbali ni kama vile kuelewa matakwa ya swali, kuwa na maarifa na ujuzi katika kujieleza kwa ufasaha na weledi walio nao katika kuelewa dhana mbalimbali zinazohusiana na somo la Kiswahili. Pia taarifa hii inaonesha sababu zilizofanya wanafunzi washindwe kujibu vizuri maswali katika baadhi ya mada ikiwa ni pamoja na kushindwa kuelewa matakwa ya swali na kukosa ujuzi na maarifa ya kujieleza kwa ufasaha. Mrejesho huu utawawezesha watunga sera, viongozi wa elimu, viongozi wa shule, walimu na wanafunzi na wadau wengine kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha kiwango cha elimu na ufaulu wa wanafunzi katika mitihani yote inayoendeshwa na Baraza la Mitihani.

Baraza la Mitihani litakuwa tayari kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na wadau mbalimbali wa elimu ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kupata ufumbuzi wa dosari zilizoainishwa katika taarifa hii.

Mwisho, Baraza la Mitihani linatoa shukrani kwa Maafisa Mitihani na walimu wa somo la Kiswahili kwa ujumla kwa ushiriki wao katika kuiandaa taarifa hii. Tunapenda pia kutoa shukrani za dhati kwa wafanyakazi wa Idara ya Uchapaji na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa ushiriki wao katika kuikamilisha taarifa hii.

Dr. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua ufaulu wa wanafunzi waliopimwa wa Kidato cha Pili mwaka 2015 kwa lengo la kutoa mrejesho kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali katika upimaji wa somo la Kiswahili. Upimaji wa somo la Kiswahili ulikuwa na maswali matano (5) yaliyogawanyika katika sehemu A *Ufahamu*, B *Utumizi wa Lugha na Usahihi wa Maandishi*, C *Sarufi,* D *Fasihi Simulizi* na E *Insha/Utungaji*. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kutoka katika sehemu A hadi E.

Upimaji wa Kiswahili Kidato cha Pili mwaka 2015 ulifanywa na jumla ya wanafunzi **356,056** kati ya wote waliojiandikisha kufanya mitihani ambapo wavulana ni **178,453** na wasichana ni **184,634.** Ufaulu wa wanafunzi kwa ujumla katika upimaji huu ulikuwa mzuri kwani kiwango cha ufaulu kilikuwa asilimia **86.34** kwa wanafunzi wote waliofanyiwa upimaji huo.

Taarifa hii inachambua maswali yaliyojibiwa vizuri na wanafunzi na yale yaliyojibiwa vibaya ili kukuza ufanisi hasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika kiwango cha elimu ya sekondari. Sampuli za majibu ya wanafunzi zimeambatishwa ili kuonesha kilichotarajiwa na watahini na kile kilichofanywa na wanafunzi.

Uchambuzi huu umezingatia viwango vya ufaulu kwa kuvigawa katika sehemu kuu tatu za ufaulu ambazo ni vizuri, wastani na hafifu. Ufaulu mzuri ulianzia alama 50 hadi 100, wastani alama 30 hadi 49 na ufaulu hafifu alama 0 hadi 29.

Aidha, uchambuzi huu unalenga kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu katika kutekeleza mkakati mzima wa matokeo makubwa sasa katika elimu kwa vizazi vya sasa na vizazi vijavyo. Kwa kuzingatia Sera ya Elimu ya Tanzania inayosema Elimu ya Awali hadi Kidato cha Nne ni elimu ya msingi, hivyo wanafunzi walioanza Kidato cha Kwanza wanatakiwa waweze kufika Kidato cha Nne.

## 2.0 TATHIMINI KWA KILA SWALI

### 2.1 Sehemu A: Ufahamu

Sehemu hii ambayo inahusu kifungu cha habari ambacho kilikuwa na swali 1 wanafunzi walipaswa kukisoma kifungu hicho na kisha kujibu maswali yaliyofuata. Kifuatacho ni kifungu cha habari walichopewa wanafunzi.

*Wakati wa ukoloni mabepari wa Kijerumani walianzisha kilimo cha pamba huko Kusini mwa Tanzania. Waliwalazimisha Wamatumbi kufanya kazi katika mashamba yao. Pamba iliyopatikana ilipelekwa Ujerumani. Kama anavyosema kibarua mmoja aliyeteswa na mabepari hao, "Wakati wa kilimo kulikuwa na dhiki sana. Sisi vibarua tuliokamatwa tulikaa mstari wa mbele, tukilima. Nyuma yetu kulikuwa na* ***mnyapara****, kazi yake kutupiga kwa* ***mijeledi****. Nyuma ya mnyapara alikuwepo jumbe, na kila jumbe alisimama nyuma ya watu hamsini. Na nyuma ya majumbe alisimama Bwana Kinoo mwenyewe. Lo! Hapo shuhudia kifo."*

*Mjerumani alipofika nchini akaamrisha Wamatumbi kulipa kodi. Watu walimjibu, "Hudai kitu. Hatuna deni kwako. Ikiwa wewe mgeni unataka kukaa nchi hii basi ni lazima wewe utuombe sisi. Na sisi tutakuambia utoe* ***sadaka*** *kwa Miungu wetu. Wewe utatoa chochote na sisi tutaifanyia karamu Miungu kwa niaba yako; tutakupa ardhi na wewe utakuwa na mahali pa kukaa. Lakini siyo sisi wenyeji tukupe wewe sadaka. Hilo haliwezekani hata kidogo."*

*Juu ya dhiki zote walizopata yaani dhiki ya njaa, dhiki ya maonevu, dhiki ya kulimishwa na kupigwa, watu* ***walistahimili*** *wakavumilia kwa sababu hawakuweza kupigana, kwani hawakuwa na umoja. Vilevile walijua kuwa nguvu ya Mjerumani ilikuwa kubwa. Wakangoja.*

*Katika mwaka wa 1904 akaja* ***mtume****, jina lake Kinjeketile. Karibu na kwao Ngarambe kulikuwa na bwawa la maji katika kijito cha Mto Rufiji. Kinjeketile alipandwa na pepo aitwaye Hongo, aliyekuwa akikaa katika bwawa hilo.*

*Kinjeketile aliwafundisha Waafrika maana ya umoja, akawapa moyo kwa nguvu ya maji. Waafrika wakawa na*

*umoja na nguvu. Watu wengi waliosikia jina lake walikuja kumuunga mkono.*

### 2.1.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali lilihusu mada ya *Ufahamu* na lililenga kupima ufahamu wa mwanafunzi. Swali lilimtaka mwanafunzi kusoma kifungu cha habari kisha kujibu maswali yaliyofuata. Maswali hayo yalikuwa na vipengele (a) hadi (e) na kipengele (f) kilihusu mada ya ufupisho. Swali hili lilikuwa na alama 15.

Kipengele (a) kilimtaka mwanafunzi kuandika kichwa cha habari kinachofaa na kisichozidi maneno matano. Kipengele (b) kilimtaka mwanafunzi kueleza wazo kuu la kifungu cha habari, kipengele (c) kilimtaka mwanafunzi aandike mambo matatu yanayothibitisha kwamba Wamatumbi waliteswa. Kipengele (d) kilimtaka mwanafunzi aeleze maana ya maneno kama yalivyotumika katika kifungu cha habari, kipengele (e) kilimtaka mwanafunzi kueleza mambo mawili aliyojifunza kutokana na habari aliyosoma na kipengele (f) kilimtaka mwanafunzi kufupisha aya ya kwanza hadi ya tatu kwa maneno yasiyozidi arobaini (40). Jedwali Na 1 linaonesha ufaulu wa wanafunzi kiidadi na kiasilimia.

**Jedwali 1: Ufaulu wa Wanafunzi Kiidadi na kwa Asilimia**

| **Alama** | **0.0 - 4.0 Hafifu** | **4.5 - 7.0 Wastani** | **7.5 -15.0 Mzuri** | **Waliofanya** |
|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 80957 | 157591 | 124543 | 363093 |
| **Asilimia** | 22.3 | 43.4 | 34.3 | 100.0 |

Asilimia 22.3 ya wanafunzi waliofanya upimaji walipata alama 0 hadi alama 4, asilimia 43.4 walipata alama 4.5 hadi alama 7.0 na waliopata alama za juu kuanzia alama 7.5 hadi 15 walikuwa ni asilimia 34.3.

Sababu za wanafunzi (34.3%) kupata alama za juu ni pamoja na kuweza kuhusisha kifungu cha habari walichosoma na maswali waliyoulizwa. Wanafunzi hao waliweza kuandika kichwa cha habari kilivyotakiwa pamoja na kujibu vipengele vingine kwa usahihi. Kielelezo 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele vyote vya swali kutokana na maarifa na uelewa aliokuwa nao kuhusu mada ya *Ufahamu* baada ya kusoma kifungu cha habari na kukielewa.

**Kielelezo 1.1**

(a) Andika kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyosoma kisichozidi maneno matano.


ENZI ZA UKOLONI

(b) Eleza wazo kuu linalojitokeza katika habari uliyoisoma.

Wazo kuu ni ukoloni katika habari niliyosoma.

(c) Ni mambo gani yanayothibitisha kwamba ni kweli Wamatumbi waliteswa? Taja mambo matatu.

(i) Kulazimishwa kufanya kazi katika mashamba yao
(ii) Kuamrishwa kulipa kodi
(iii) Kupigwa mijeledi



(d) Toa maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu cha habari ulichosoma.

(i) Mnyapara... ni msimamizi anayeongoza kitu/watu.

(ii) Mijeledi... ni kama fimbo kutumika kuadhibu.

(iii) Walistahimili... ni kujikaza na kuvumilia yote.

(iv) Sadaka... ni shukrani atoayo mtu baada ya kupata mafanikio ya kitu fulani alichokuwa akiomba

(v) Mtumwa... ni mtu mwenye imani...

(e) Ni mambo gani mawili unayojifunza kutokana na habari hii?

(i) Umoja ni nguvu na utengano ni dhaifu

(ii) Mvumilivu hula mbivu

(f) Fupisha aya ya kwanza hadi ya tatu kwa maneno yasiyozidi 40.


Wakoloni wa kijerumani walianzisha kilimo cha pamba huko kusini mwa Tanzania. Walikamatwa vibarua kutoka hapa nchi na kufanyishwa kazi mjerumani alipofika nchi ni akaamrisha wanachumbi kulipa kodi juu ya vichiki walizopata lakini walistahimili wakavumilia.

Kielelezo 1.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeelewa kifungu cha habari na hivyo kuweza kutoa majibu ya maswali ya kifungu hicho kwa usahihi.

Aidha, asilimia 22.3 ya wanafunzi walishidwa kujibu swali hili na kupata alama chini ya wastani. Miongoni mwao, wanafunzi wachache (1.0%) walishindwa kujibu vipengele vyote kwa usahihi na hivyo kupata alama 0. Wanafunzi hao walishindwa kujibu hata kipengele (a) kilichomtaka mwanafunzi kuandika kichwa cha habari waliyosoma ambacho kilitakiwa kisizidi maneno matano. Baadhi ya wanafunzi hao waliandika kichwa cha habari ambacho sio sahihi. Wanafunzi wengine waliandika kwa herufi ndogo,

jambo ambalo liliwakosesha alama kutokana na kutokuzingatia kanuni za uandishi wa kichwa cha habari ambazo husisitiza kuandikwa kwa usahihi na kwa herufi kubwa. Katika baadhi ya vipengele wanafunzi hao walishindwa kuandika maana ya maneno kama yalivyotumika katika kifungu cha habari, badala yake waliandika maelezo ambayo hayaendani na matakwa ya swali. Kielelezo 1.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi ambaye ameshindwa kuelewa maudhui katika kifungu cha habari alichosoma.

**Kielelezo 1.2**



(a) Andika kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyosoma kisichozidi maneno matano. walati wa ukoloni mabepari


(b) Eleza wazo kuu linalojitokeza katika habari uliyoisoma. Mirumani alipofika nchini alaamrisha wamatumbi kulipa kodi

(c) Ni mambo gani yanayothibitisha kwamba ni kweli Wamatumbi waliteswa? Taja mambo matatu.

(i) Kipa kodi

(ii) watu wali

(iii) "Hudai Kitu


(d) Toa maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu cha habari ulichosoma.

(i) Mnyapara... Kazi yake kutupiga kwa mijeledi

(ii) Mijeledi... Nyumba ya mnyapara alikuwa mjumbe

(iii) Walistahimili... walo uima kwa sababu hawakuwe za kupiga


(iv) Sadaka... kwa mungu wetu

(v) Mtume... jina lake kilijekitile

(e) Ni mambo gani mawili unayojifunza kutokana na habari hii?

(i) mjerumani alipofika nchini akaamrisha kulipa kodi

(ii) juu ya dhiki zote walizopata yaani dhiki ya njaa


(f) Fupisha aya ya kwanza hadi ya tatu kwa maneno yasiyozidi 40.

wakati wa ukoloni wa kijerumani walianzisha kilimo cha pamba yao pamba ikipatikana ili peleka kwa kijerumani kama anavyosema kibarua moja aliyepewa mshahara wa mbali ulikuwa kilima nyumba yetu kuu.

Kielelezo 1.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kuelewa matakwa ya swali na hivyo kushindwa kujibu kwa usahihi.


## 2.2 Sehemu B: Matumizi ya Lugha na Usahihi wa Maandishi

### 2.2.1 Swali la 2: Usahihi wa Tungo na Rejesta

Swali hili linahusu mada ya *Matumizi ya Lugha na Usahihi wa Maandishi*. Swali lililenga kupima matumizi na lilimtaka mwanafunzi kutumia lugha katika miktadha mbalimbali. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15 katika vipengele (a) hadi (c), ambapo kipengele (a) kilimtaka mwanafunzi

kuandika KWELI kwa kauli iliyo sahihi, au SIO KWELI kwa kauli isiyo sahihi katika sentensi alizopewa.

Kipengele (b) kilimtaka mwanafunzi kuandika tungo alizopewa kwa usahihi na kipengele (c) kilimtaka mwanafunzi aandike mifano ya kauli zinazoonesha miktadha ya rejesta mbalimbali.Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika swali hili na ufaulu wake kiasilimia umewasilishwa vizuri katika Chati Na 1 kwa kuonesha ufaulu hafifu, wastani na mzuri.




**Chati 1:** Ufaulu wa Wanafunzi kwa asilimia

Asilimia 92.6 ya wanafunzi waliofanya upimaji waliweza kujibu kwa usahihi na kupata alama 7.5 hadi 15. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Mwanafunzi aliyepata alama zote aliweza kubainisha kauli ambazo ni sahihi kwa kuandika KWELI na kauli isiyo sahihi kwa

kuandika SIO KWELI katika kipengele (a). Aidha, mwanafunzi huyo aliweza kubaini usahihi wa tungo katika kipengele (b) na katika kipengele (c) mwanafunzi aliweza kuandika kauli zinazoonesha muktadha wa rejesta alizopewa. Kielelezo 2.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu swali la 2 kwa usahihi na kupata alama 15.

**Kielelezo 2.1**

2. (a) Kwa kauli zifuatazo andika **KWELI** kwa kauli iliyo sahihi au **SIO KWELI** kwa kauli isiyo sahihi.

(i) Kazi ya fasihi ni moja tu na ni ile ya kuelimisha jamii. SIO KWELI

(ii) Kiunganishi ni neno ambalo huunganisha dhana mbili tu.
SIO KWELI

(iii) Elekeza, shikilia, shikamana, maelekezo, mshikamano, tolewa, nitakutolea ondokeni ni maneno yaliyoundwa kutokana na mnyumbuliko. KWELI

(iv) Methali ni usemi wenye pande mbili. KWELI

(v) Kitendawili ni aina ya fumbo lisilotumia lugha ya picha lakini hudai jibu. KWELI

(b) Andika tungo zifuatazo kwa usahihi:

(i) Mwalimu mkuu amewakilisha mada katika mkutano.
Mwalimu mkuu amewasilisha mada katika mkutano

(ii) Nilikwenda mjini nikamkutana Maria.

Nilienda mjini nikakutana na Maria.

(iii) Habarini zenu mabibi na mabwana.

Habari zenu Mabibi na Mabwana.

(iv) Kila siku nafanyaga kazi.

Kila siku nafanya kazi.

(v) Kwa kuwa sina gari nitakwenda na miguu.

Kwa kuwa sina gari nitaenda kwa miguu.

(c) Andika mifano ya kauli zinazoonesha muktadha wa rejesta zifuatazo;

(i) Hotelini... Niletee wali nyama.

(ii) Mahakamani.. Mtuhumiwa kesi ni yako

(iii) Dukani.... Daftari unauza bei gani

(iv) Darasani... Kaniletee Chati.


(v) Hospitalini.. Hizi dawa kunywa kutwa mara tatu.

Kielelezo 2.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu swali vizuri kwa kubaini usahihi wa tungo na matumizi ya rejesta husika.

Aidha, asilimia 5.5 ya wanafunzi waliofanya swali hili walipata alama 4.5 hadi alama 7 ambazo ni alama za wastani. Wanafunzi hawa waliweza kujibu baadhi ya vipengele vya swali hili kwa usahihi. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliweza kujibu vizuri vipengele (b) na (c) na

wengine walijibu vipengele (a) na (b) kwa usahihi. Kielelezo 2.2 kinaonesha sampuli ya mwanafunzi aliyejibu vizuri vipengele (b) na (c), ijapokuwa katika kipengele (b) hakujibu kipengele (i).

**Kielelezo 2.2**


(b) (i) ..............................................................................

(ii) Nilikwenda mjini nikamkutana Maria.
Nilikwenda mjini nikakutana na Maria....

(iii) Habarini zenu mabibi na mabwana.
Habari zenu mabibi na mabwana...

(iv) Kila siku nafanyaga kazi.
Kila siku huwa nafanya kazi.....

(v) Kwa kuwa sina gari nitakwenda na miguu.
Kwa kuwa sina gari nitaenda kwa miguu.........

(c) Andika mifano ya kauli zinazoonesha muktadha wa rejesta zifuatazo;
(i) Hotelini... Nipatie wali kuku na nyama ya ng'ombe.
(ii) Mahakamani.. Kamata huyo na umweke ndani.
(iii) Dukani.. Nipatie sukari kilo moja na mchele kilo mbili.
(iv) Darasani.. Leo tutajifunza usafi wa mwili.

Kielelezo 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele (b) na (c) japo sehemu nyingine aliongeza maneno ambayo hayakuwepo kwenye kipengele (b). na pia hakuweza kujibu kipengele kidogo cha (b) (i).

Wanafunzi wachache sana (1.8%) walipata chini ya alama 4.5 ambapo miongoni mwao asilimia 0.1 walipata alama 0. Wanafunzi hao walishindwa kujibu baadhi ya vipengele kwa usahihi na hivyo kupata alama za chini ya wastani kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu matumizi ya lugha kwa ujumla. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja katika

kipengele (b) alishindwa kufuata maelekezo ya swali yaliyomtaka kuandika tungo kwa usahihi, badala yake alijibu kwa kutaja aina za tungo ambazo pia hazikuwa majibu sahihi. Wanafunzi wengine walishindwa kubainisha kauli sahihi na zisizo sahihi na hata kushindwa kutaja rejesta kulingana na muktadha waliopewa. Kielelezo 2.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kipengele (b) kwa kutokufuata maelekezo ya swali.

**Kielelezo 2.2**

(b) Andika tungo zifuatazo kwa usahihi:

(i) Mwalimu mkuu amewakilisha mada katika mkutano.
......tungo......shurutia.........

(ii) Nilikwenda mjini nikamkutana Maria.
......tungo......shurutia......

(iii) Habarini zenu mabibi na mabwana.
...tungo......changamano.....

(iv) Kila siku nafanyaga kazi.
...tungo......tegemezi...........

(v) Kwa kuwa sina gari nitakwenda na miguu.
......tungo..................changamano......

Kielelezo 2.2 ni mfano wa majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kuandika tungo kwa usahihi na badala yake aliandika aina za tungo.

## 2.3 Sehemu C: Sarufi

### 2.3.1 Swali la 3: Aina za Maneno na Uambishaji

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno na Uambishaji* na lililenga kupima majazi ya utambuzi ngazi ya uchambuzi. Swali lilimtaka mwanafunzi katika kipengele (a) kunyambua maneno aliyopewa na kuunda maneno manne kwa kila neno. Kipengele (b) kilimtaka mwanafunzi kutumia


maneno aliyopewa (nomino) kutunga sentensi moja kwa kila neno na kipengele (c) kilimtaka mwanafunzi kuonesha kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu katika sentensi alizopewa. Jedwali Na 2 linaonesha ufaulu wa wanafunzi kiidadi na kwa asilimia.

**Jedwali 2: Ufaulu wa Wanafunzi Kiidadi na kwa Asilimia**

| Alama | 0.0 - 4.0 Hafifu | 4.5 - 7.0 Wastani | 7.5 - 15.0 Mzuri | Waliofanya |
|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 53229 | 79983 | 229879 | 363093 |
| **Asilimia** | 14.7 | 22.0 | 63.3 | 100.0 |

Asilimia 63.3 ya wanafunzi waliojibu swali hili waliweza kulijibu vizuri na kupata zaidi ya nusu ya alama zote zilizopangwa kwa swali hilo na kuweza kupata alama 7.5 hadi 15. Wanafunzi waliopata alama zote 15 waliweza kujibu vipengele vyote vya swali hili kwa usahihi kama vile kunyambua maneno waliyopewa, kutunga sentensi kwa kutumia nomino walizopewa na kubainisha vitenzi visaidizi vilivyotumika sambamba na vitenzi vikuu katika sentensi walizopewa. Kielelezo 3.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu swali hili vizuri na kupata alama zote.

**Kielelezo 3.1**


3. (a) Nyumbua maneno yafuatayo na kuunda maneno manne kwa kila neno

(i) Angalia Angaliana angaliwa
Angalieni waangaliwa

(ii) Chukua Chukuliwa Chukuliana
Chukulieni waChukue

(iii) Oga Ogeni
Ogeshana Ogeshwa

(iv) Kata Katisha Katishwa
Katishana Katiwa

(v) Omba Ombwa Ombeana
Ombewa Ombana

(b) Tumia maneno yafuatayo kama nomino na utunge sentensi moja kwa kila neno:

(i) Starehe ... Starehe ni mbaya sana.

(ii) Ukweli ... Ukweli ni kuamba Asha ni mwizi.

(iii) Utaalamu ... Utaalamu wake ni wa kweli

(iv) Umoja ... Umoja ni kauli mbiu yetu.

(v) Uzembe ... Uzembe ni kikwazo cha maendeleo.

(vi) Ukarimu ... Ukarimu ni nguzo ya taifa letu

(vii) Ushujaa ... Ushujaa ni sifa yetu sote Watanzania

(viii) Upweke ... Upweke ni mbaya na pia unauma.

(ix) Upendo ... Upendo ni mzuri kuliko Rehema.

(x) Furaha ... Furaha ndio nguzo kwa kwetu.

(c) Kitenzi kikuu huweza kutumika sambamba na kitenzi kingine kukamilisha sentensi. Katika sentensi zifuatazo bainisha vitenzi vilivyotumika. Sentensi ya kwanza ni mfano:

(i) Aliyekuja atasafiri kesho.

TS T

(ii) Mgeni wangu amekwisha kuwasili.

... TS ... T ...

(iii) Amina hakutaka kumuudhi.

... TS ... T ...

(iv) Mafundi wangali wanashona viatu.

... TS ... T ...

(v) Wataendelea kumsubiri hadi kesho.

... TS ... T ...


(vi) Gari lilikuwa limeharibikia mlimani Kitonga.

... TS ... T ...

Kielelezo 3.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kubainisha kitenzi kikuu na kitenzi kisaidizi kwa usahihi na kupata alama 15.

Licha ya baadhi ya wanafunzi kujibu swali hili vizuri na kupata alama zote 15, asilimia 14.7 ya wanafunzi waliojibu swali hili walipata alama chini ya wastani, kutokana na kushindwa kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele. Miongoni mwa wanafunzi hao asilimia 1.1 walishindwa kujibu swali hili na kupata alama sifuri kama Kielelezo 3.2 kinavyoonesha.

**Kielelezo 3.2**



3. (a) Nyumbua maneno yafuatayo na kuunda maneno manne kwa kila neno.

(i) Angalia Angalia mama. angalia Zawadi.
Angalia mti. angalia kitu

(ii) Chukua Chukua kitu. chukua Zawadi.
Chukua chakula. Chukua lambilambi.

(iii) Oga oga bafuni. oga pekeyako.
oga maji oga mtoni.

(iv) Kata Kata kupepea mzigo. Kata mti
Kata ya maji. Kata kitu.

(v) Omba omba msaada. omba mungu.
omba akusamehe. omba kitu

(b) Tumia maneno yafuatayo kama nomino na utunge sentensi moja kwa kila neno:

(i) Starehe ..mashfrfht........

(ii) Ukweli ..wakaliuliopo........

(iii) Utaalamu ..wakaliuliopita........

(iv) Umoja ......nafsi ya pili umoja........

(c) Kitenzi kikuu huweza kutumika sambamba na kitenzi kingine kukamilisha sentensi. Katika sentensi zifuatazo bainisha vitenzi vilivyotumika. Sentensi ya kwanza ni mfano:

(i) Aliyekuja atasafiri kesho.

TS T

(ii) Mgeni wangu amekwisha kuwasili.

W E T V

(iii) Amina hakutaka kumuudhi

N T V

(iv) Mafundi wangali wanashona viatu.

N V T N

(v) Wataendelea kumsubiri hadi kesho.

E V V E

(vi) Gari lilikuwa limeharibikia mlimani Kitonga.

N T T W N

Kielelezo 3.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi kutokana na kushindwa kufuata maelekezo ya swali.


Hata hivyo, asilimia 22.0 ya wanafunzi waliojibu swali hili walipata alama 4.5 hadi alama 7.0 ambazo ni alama za wastani. Watahiniwa hao walishindwa kujibu baadhi ya vipengele vya swali kwa usahihi kwa kuwa walikosa maarifa kuhusu aina za maneno na uambishaji. Baadhi ya wanafunzi hao walishindwa kunyambua maneno waliyopewa kwa kuunda maneno mengine manne. Aidha, wanafunzi wengine walishindwa kutunga sentensi kutokana

na nomino walizopewa na kushindwa kubainisha vitenzi vikuu na vitenzi visaidizi katika sentensi walizopewa.

## 2.4 Sehemu D: Fasihi Simulizi

### 2.4.1 Swali la 4: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na lilikuwa na vipengele (a), (b) na (c) vilivyobeba jumla ya alama 40. Swali lililenga kupima majazi ya utambuzi ngazi ya maarifa. Katika kipengele (a) swali lilimtaka mwanafunzi kueleza kwa kifupi maana ya dhana mbalimbali za fasihi simulizi, Kipengele (b) kilimtaka mwanafunzi kukamilisha methali kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi na kipengele (c) kilimtaka mwanafunzi kusoma shairi na kujibu maswali yaliyofuata. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika swali hili na ufaulu wake kwa asilimia umefafanuliwa vizuri katika Chati Na 2 kwa kuonesha ufaulu hafifu, wastani na mzuri.




**Chati 2:**Ufaulu wa Wanafunzi kwa Asilimia

Asilimia 61.5 ya wanafunzi waliojibu swali hili walipata chini ya alama 12 ambazo ndizo alama za wastani. Swali hili ndilo lililojibiwa vibaya sana na wanafunzi wengi kutokana na wanafunzi hao kushindwa kueleza kwa kifupi dhana mbalimbali za Fasihi Simulizi walizopewa. Dhana hizo ni kama vile, shairi ambalo ni mpangilio wa maneno kwenye tungo kwa utaratibu maalum wa silabi, lugha ya mkato na ya kitamathali, vichekesho ambavyo ni mpangilio wa maneno wenye utendekaji, ngonjera ambazo ni mpangilio wa beti za mashairi ya kujibizana unaoambatana na utendaji. Visasili ni hadithi fupi zenye kuelezea vyanzo au asili ya tabia/maumbo yanayohusiana na maumbile ya watu, wanyama na pia miti. Mapingiti ni aina ya mashairi yasiyofuata mtiririko wa vina na mizani. Aidha, wapo wanafunzi walioshindwa kukamilisha methali walizopewa kwa usahihi, jambo linalodhihirisha kuwa wanafunzi hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu fasihi simulizi na tanzu zake. Kielelezo 4.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi na hivyo kupata alama 0.

**Kielelezo 4.1**

4. (a) Eleza kwa kifupi maana ya dhana zifuatazo:

(i) Shairi....Ni kipera cha fasihi simulizi kinacho husu mashiri....

(ii) Vichekesho.......................................................

(iii) Ngonjera....Ni mashairi yanayo chekesha ili kutoa ujumbe....

(iv) Visasili.......................................................

(v) Mapingiti....Ni maneno yanayo tumika kuonesha Mahali....

(b) Jaza nafasi iliyoachwa wazi kukamilisha methali zifuatazo:

(i) Samaki mkunje ....Hali wali mkavu.............. ....

(ii) .......Nyapara...........njaa mwana malegeza.

(iii) ....Maji......................hutanda na kuyeyuka.

(iv) Ajidhaniaye kasimama....kupenda......chupuchupu..

(v) .........Mwizi......... .... usiilalie mlango wazi.

Kielelezo 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi vipengele (a) na (b).

Katika kipengele (c) wanafunzi hao walishindwa kulielewa shairi walilopewa, hivyo kushindwa kujibu maswali yatokanayo na shairi hilo kulingana na maelekezo ya swali. Kielelezo 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi maswali hayo yatokanayo na shairi hilo. Lifuatalo ni shairi walilopewa wanafunzi:

*Mwanafunzi **ikibali**, mbele ya wako mwalimu,*
*Katika siku si mbali, utakuwa aalimu,*
*Kijitia **baradhuli**, baadaye ulaumu,*
*Mbele ya wako mwalimu, mwanafunzi ikibali.*

*Usijifanye kiburi, kujifanya **chakaramu**,*
*Hiyo wanaita shari, ndani yake ina sumu,*
*Hivi hauna habari, heshima kitu adimu,*
*Mbele ya wako mwalimu, mwanafunzi ikibali.*

*Katika hii sayari, namba moja ni elimu,*
*Usiipate sufuri, kisha hapo ulaumu,*
*Maisha haya safari, mwana ujenge timamu,*
*Mbele ya wako mwalimu, mwanafunzi ikibali.*

*Ni walezi mashuhuri, hivyo wana umuhimu,*
*Wameishika nambari, kutokana na kalamu,*
*Usimwendeshe **chuchuri**, uidumishe nidhamu,*
*Mbele ya wako mwalimu, mwanafunzi ikibali.*

*Mwalimu baba na mama, hilo wazi ufahamu,*

*Hivyo tazama ndarama, zisisababishe* ***ghamu****,*
*Neno hili ni la zama, shika nakupa jukumu,*
*Mbele ya wako mwalimu, mwanafunzi ikibali.*

*Sitapenda kukuchosha, kwa mengi kukushutumu,*
*Nakutakia maisha, ya shule yenye utamu,*
*Ili upate* ***bashasha****, na mema* ***kutakadamu****,*
*Mbele ya wako mwalimu, mwanafunzi ikibali.*

**Kielelezo 4.2**

(i) Mtunzi wa shairi hili anatoa ujumbe gani?

...Kwa kutoa msisitizo kwa wanafunzi juu ya kusoma...

(ii) Ni mambo gani matatu ambayo mwanafunzi unatakiwa kuyaepuka kama yalivyoelezwa katika shairi ulilosoma?

...① Kuepuka kiburi...
...② kuepuka shari na ulania...
...③ kuepuka uchakarechakare...

(iii) Bainisha kituo bahari katika shairi ulilosoma.

...Mbele ya mwanafunzi...

(iv) Bainisha vina vya kati na vya mwisho vya shairi ulilosoma.

...i na wako...

(v) Mshairi ana maana gani anaposema, "Neno hili ni la zama, shika nakupa jukumu."

...Ana maana kwa ni kuyashika maneno anayo sema na kuyafanyia kazi...

(vi) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi ulilosoma;

- Ikibali ......ni umuhimu................
- Baradhuli....Ni ujanja.....................
- Kutakadamu ....Ni kuzingatia jambo ....fulani.
- Chuchuri.....ni kufanya kitu ovyo ovyo bila maelekeo
- Bashasha ....ni maendeleo au jambo ya kitu fulani

Kielelezo 4.2 ni majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali lote kwa usahihi na kupata alama sifuri.

Licha ya swali hili kujibiwa vibaya na wanafunzi wengi, wanafunzi wachache, asilimia 6.0 waliweza kulijibu kwa kiwango kizuri na kuweza kupata alama 20 hadi 40. Wanafunzi hao waliweza kueleza mambo muhimu yaliyotokana na shairi hilo. Aidha, wanafunzi hao waliweza kubainisha kituo bahari na kueleza maana sahihi za maneno waliyopewa, ambayo yalitumika katika shairi walilosoma. Kielelezo 4.3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi.

**Kielelezo 4.3**

(i) Mtunzi wa shairi hili anatoa ujumbe gani?
Wanafunzi wanatakiwa wawaheshimu walimu wao. mfano anaposema mwanafunzi ikibali, mbele ya wako mwalimu.

(ii) Ni mambo gani matatu ambayo mwanafunzi unatakiwa kuyaepuka kama yalivyoelezwa katika shairi ulilosoma?
1. Aepuke kiburi
2. kuepuka uchakaramu
3. Aepuke ubaradhuli

(iii) Bainisha kituo bahari katika shairi ulilosoma.
Mbele ya wako mwalimu, mwanafunzi ikibali

(iv) Bainisha vina vya kati na vya mwisho vya shairi ulilosoma.
Ubeti wa kwanza ni vya kati ni "Li" na vya ~~mis~~ mwisho ni "mu" ubeti wa pili vya kati ni "ri" na vya mwisho ni "mu", "ti" na mu, "ti" na mu", "ma" na "mu", "sha" na mu".

(vi) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi ulilosoma;


- Ikibali ...Ni kile kitendo cha kutii au kuheshimu jambo.
- Baradhuli...Ni ile hali ya kuwa na kiburi.
- Kutakadamu ...Ni kitendo cha kupata kitu.
- Chuchuri...Ni hali ya kutokuwa na nidhamu
- Bashasha ...furaha isiyo kifani yaani furaha kubwa.

Kielelezo 4.3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu swali hili kwa kiwango kizuri ijapokuwa ameshindwa kueleza maana ya baadhi ya maneno kwa usahihi.

## 2.5 Sehemu E: Uandishi wa Insha/Utungaji.

### 2.5.1 Swali la 5: Uandishi wa Barua za Kirafiki

Swali lilihusu mada ya *Utungaji* katika kipenglele cha uandishi wa barua ya kirafiki na lilijibiwa na wanafunzi 363,045 kati ya 363,093 waliofanya upimaji. Swali lililenga kupima majazi ya utambuzi katika ngazi ya utungaji na lilimtaka mwanafunzi kuandika barua ya kirafiki/kindugu kumjulisha shangazi yake kwamba angemtembelea. Chati Na 3 inaonesha uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi kwa mada na kwa asilimia.




**Chati 3:** Ufaulu wa Wanafunzi kwa Asilimia

Asilimia 28.7 ya wanafunzi waliojibu swali hili walipata alama za wastani yaani 4.5 hadi alama 7.0. Sababu za wanafunzi hao kupata alama za wastani ni kushindwa kuzingatia baadhi ya kanuni za uandishi wa barua. Miongoni mwa wanafunzi hao, wapo waliosahau kuweka tarehe, kuanza na salamu na pia hawakuzingatia kuandika anwani upande wa kulia. Aidha, wanafunzi wengine waliandika anwani mbili kama vile ni barua rasmi, hivyo kutokuzingatia kanuni za uandishi wa barua ya kindugu/kirafiki. Kielelezo 5.1 kinaonesha swali lilivyokuwa na sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kuandika barua ya kirafiki kwa kutokufuata baadhi ya kanuni za uandishi wa barua na pia kutokuzingatia maelekezo ya swali.

**Kielelezo 5.1**

5. Unatarajia kwenda kumtembelea shangazi yako aitwaye Nakijwa aishiye Ikwiriri Rufiji. Andika barua kwa shangazi kumjulisha makusudio yako. Jina lako liwe Jaja Okwi, Shule ya Sekondari Ndorwe, S.L.P 1534. Kilomeni. Mwanga.

SHULE YA SECONDARI NDORWE,
S.L.P 1534,
KILOMENI MWANGA,
22 DECEMBA 2015.

MPENDWA SHANGAZI,
S.L.P 1534,
IKWIRIRI RUFIJI.


Salamu sana shangazi nina mwanafunzi wazima wa afya sana nimi ni mzima sana nashukuru sana jina langu ni Jaja Okwi Shule ya Sekondari Ndorwe. na shukuru sana Mungu awe na sisi sote nami nitakuunga nawe salimia wako mtiifu

DONARD...

Kielelezo 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika barua yenye anwani mbili, jina la mwandishi tofauti na lilitolewa na pia hakuzingatia jambo ambalo lilitakiwa kuandikwa katika barua hiyo ya kirafiki.

Aidha, asilimia 28.7 ya wanafunzi waliojibu swali hili walishindwa kuandika barua ya kirafiki/kindugu na badala yake waliandika simu ya maandishi badala ya barua ya kirafiki, kutokana na kuchanganya maarifa ya barua ya kirafiki na aina nyingine za barua kama vile simu ya maandishi. Miongoni mwa wanafunzi hao, asilimia 19.2 walipata alama 0 kwa kushindwa kuandika barua ya kirafiki na wanafunzi wengine waliacha swali hili wazi bila kuandika chochote. Kielelezo 5.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 5.2**


NAKISA IKWIRIRI RUFIJI NATAKA KUJA KUWATEMBELEA
MIMI JAJA OKWI SEKONDARI NDORWE S.L.P 1534

Kielelezo 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika simu ya maandishi badala ya barua ya kirafiki/kindugu.

Hata hivyo, asilimia 42.6 ya wanafunzi waliofanya swali hili waliweza kuandika barua ya kirafiki/kindugu na kupata kati ya alama 7.5 hadi 15. Ufaulu huu unadhihirisha kuwa stadi ya uandishi wa barua ya kindugu/kirafiki ilieleweka vizuri kwa wanafunzi hao. Wanafunzi hao waliweza kuzingatia muundo wa barua ya kirafiki kwa kuandika anwani ya mwandishi upande wa kulia juu na chini yake kuandika tarehe ya uandishi wa barua hiyo. Aidha, wanafunzi hao walikuwa na mwanzo wa barua wenye salamu, kiini/dhumuni/lengo la barua, mwisho wa barua wenye jina la mwandishi kama lilivyoelekezwa. Wanafunzi hao walizingatia pia taratibu za uandishi. Kielelezo 5.2 ni mfano wa majibu mazuri ya mwanafunzi aliyekidhi taratibu za uandishi wa barua ya kirafiki/kindugu.

**Kielelezo 5.3**

UANDISHI WA BARUA YA KIRAFIKI

SHULE YA SEKONDARI NDORWE,
S.L.P. 1534,
KILOMENI, MWANGA.
16 – 11 – 2015.

Ndugu Nakijwa,

Shikamoo shangazi, Mimi huku shuleni sijambo kabisa. Matumaini yangu wewe ni mzima pamoja na Mjomba nami pia mzima wa afya.

Shangazi yangu kusudi la barua hii ninataka kukwambia kwamba nitakuja huko nyumbani kwako kukutembelea Shangazi yangu wakati wa likizo ya mwezi wa kumi na mbili mwaka huu.

Nitakuja baada ya kumaliza mitihani yangu ya kidatu cha pili mwaka huu. Nakuomba shangazi uje kunipokea katika sitendi ya mabasi Ikwiriri, Rufiji 20-11-2015.

Wasalimie wadogo zangu wote marafiki zangu, majirani na mjomba wape taarifa kwamba mimi nitakuja kusherekea nawo sikukuu ya kirsimasi na mwaka mpya.

Tutaonana wakati na kuja nyumbani.

Ni mimi mwanao,
Tija Okwi.

Kielelezo 5.3 kinaonesha sampuli ya majibu mazuri ya mwanafunzi aliyeandika barua ya kirafiki/kindugu kwa kuzingatia muundo, kanuni na taratibu za uandishi wa barua ya kirafiki.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KWA MADA

Ufaulu wa wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi walifanya vizuri zaidi katika mada ya *Matumizi ya Lugha na Usahihi wa Maandishi* kwa asilimia 98.2 Hata hivyo, mada zingine zilizofanyika vizuri ni mada za *Ufahamu* (77.7%), *Sarufi* (85.3%) na *Utungaji* (71.3%). Aidha, ufaulu katika mada ya *Fasihi Simulizi* ulikuwa asilimia 38.5 ambao ni wa kiwango cha wastani. Ufaulu katika mada ya *Fasihi Simulizi* unaonesha kuwa wa chini zaidi ukilinganisha na ufaulu katika mada nyingine zilizotahiniwa katika upimaji huu kutokana na wanafunzi kutokuwa na uelewa, hivyo kukosa umahiri wa kutosha kuhusu mada ya *Fasihi Simulizi*. Hivyo, uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi walijibu kwa kiwango cha wastani katika mada ya *Fasihi Simulizi* kutokana na kushindwa kuelezea maana ya dhana mbalimbali, kutokukamilisha methali na kushindwa kujibu maswali yatokanayo na shairi.

Ufaulu wa wanafunzi kupitia mada mbalimbali umeainishwa katika Kiambatisho kilicho mwishoni mwa taarifa hii. Aidha, Kiambatanisho hicho kimetoa ulinganifu wa ufaulu wa mwaka 2014 na mwaka 2015. Kwa mfano, ufaulu mzuri wa mada ya *Matumizi ya Lugha na Usahihi wa Maandishi* ambayo iliongoza kwa mwaka 2014 kwa kuwa na asilimia 94.1 na mwaka 2015 mada hiyo imeongoza tena kwa asilimia 98.2. Mada ya *Fasihi Simulizi* iliyofanyika vibaya mwaka 2014 kwa kuwa na asilimia 13.8 kwa mwaka 2015 imefanyika kwa kiwango cha wastani kwa kuwa na asilimia 38.5 ikiwa ni ongezeko la asilimia 23.

Uchambuzi huu wa mada katika Upimaji wa Kidato cha Pili kwa mwaka 2015 unaonesha kuwa ufaulu ni mzuri. Hata hivyo, mkazo zaidi usisitizwe katika ujifunzaji na ufundishaji wa mada ambayo ufaulu wake umeonekana kuwa wa kiwango cha wastani ili kuwajengea wanafunzi weledi na kuwafanya wapate umahiri katika somo hili ili hatimaye kiwango cha ufaulu kiongezeke katika mada husika.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla Upimaji wa Kidato cha Pili katika somo la Kiswahili mwaka 2015 ulizingatia muhtasari wa somo la Kiswahili na maswali yote yalihusisha ngazi zote za majazi ya utambuzi, yaani maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini. Kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi kilikuwa ni kizuri ambapo wastani wa ufaulu kwa mada zote ulikuwa ni asilimia 86.34

Uchambuzi huu unaonesha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutatuliwa kama vile kutofuata maelekezo ya swali, uelewa mdogo wa mada mbalimbali na hasa mada ya *Fasihi Simulizi*. Ili kuinua zaidi kiwango cha ufaulu kwa mada za upimaji katika Upimaji wa Kidato cha Pili, jitihada zaidi inahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji ili kuwajengea wanafunzi umahiri katika kujieleza bila kikwazo chochote hasa ikizingatiwa kuwa Kiswahili ni lugha ya Taifa.

Mwisho taarifa hii ya upimaji kuhusu majibu ya wanafunzi itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili na kutoa changamoto kwa walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali. Hali hii itawafanya walimu na wanafunzi kuyaelewa makosa mbalimbali yanayosababisha ufaulu kutokuwa mzuri ili kuweza kufanya marekebisho na kuongeza ufaulu kwa miaka ijayo.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili inapendekezwa kuwa:

(a) Walimu waweke mkazo katika ufundishaji/ujifunzaji wa mada zote na hasa mada za *Fasihi Simulizi* na *Ufahamu*.

(b) Walimu wasisitize usomaji wa vitabu vya ziada au maandiko mbalimbali ili kuwajengea wanafunzi umahiri katika stadi za kusoma na kuandika.

(c) Matumizi ya lugha fasaha ya Kiswahili yasisitizwe kwa wanafunzi katika mazungumzo na maandishi yao ya kila siku ili kuboresha msamiati wa lugha ya Kiswahili.

KIAMBATISHO A

**MUHTASARI WA UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA SOMO LA KISWAHILI KWA KILA MADA**

| Na | Mada | Namba ya Swali | Asilimia ya Ufaulu (Waliopata alama 30 au zaidi) | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Utumizi wa Lugha na Usahihi wa Maandishi | 2 | 98.2 | Vizuri |
| 2. | Sarufi | 3 | 85.3 | Vizuri |
| 3. | Ufahamu na Ufupisho | 1 | 77.7 | Vizuri |
| 4. | Uandishi wa Insha/Utungaji | 5 | 71.3 | Vizuri |
| 5. | Fasihi Simulizi | 4 | 38.5 | Wastani |

**KIAMBATISHO B**

## UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA MADA NA KWA ASILIMIA KWA MWAKA 2014 NA 2015

